KISWAHILI - GRADE 5 TERM 2 CBC EXAMS 2022

Some mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswall 1-5.

(Mwalimu na wanafunzi wanajadiliana kuhusu umuhimu wa kuyatunza mazingira)

Mwalimu: Hamjambo wanafunzi?
Wanafunzi: (Wakiamka sawia) Hatujambo mwalimu, shikamoo.
Mwalimu: Marahaba (Anawaashiria wakae. Wote wanaketi na kushukuru.) Naam, leo ningependa tuzungumze kuhusu namna na umuhimu wa kuyatunza mazingira kwa hivyo...
Matayo: (Anaunyanyua mkono wake) Samahani mwalimu, mazingira ni nini?
Mwalimu: (Akitabasamu) Matayo huishi vituko! Ndilo nililotaka kueleza. Mazingira ni yale yote yanayotuzunguka. Hebu pendekezeni njia mbalimbali za kuyatunza mazingira
Manyanga: Nadhani ni vyema kukata nyasi ndefu ili kuharibu makao ya mbu.
Kaisari: Ni vyema pia kutunza vyanzo vya maji kama vile mito, chemichemi, mabwawa na maziwa.
Pendo: Nikiongezea, si vyema kutumia mbolea nyingi zaidi hasa za madukani ili tusiyaathiri maji na udongo.
Mwalimu: Nimefurahia mno michango yenu. Zipo njia nyingi za kuyatunza mazingira. Kimsingi, umuhimu wa kuyatunza mazingira ni kuwafanya viumbe waishi maisha salama.

1. Mazungumzo haya yaliandaliwa majira ya saa ngapi?
    A. Saa sita adhuhuri.
    B. Saa mbili asubuhi.
    C. Saa kumi jioni.
    D. Hatujaelezwa.
2. Ili kuonyesha heshima kuu, mwalimu alipowaamkia wanafunzi, wote
    A. walisimama ili kupokea salamu yake.
    B. walitaka kuchangia katika majadiliano
    C. walitaka kujua maana ya mazingira.
    D. walitaja umuhimu wa kuishi katika mazingira safi.
3. Ni mwanafunzi yupi aliyemkatiza mwalimu alipokuwa akiongea?
    A. Manyanga .
    B. Matayo
    C. Kaisari
    D. Pendo